# Kivuli cha Usaliti

Nyamari M. Abel

**Kivuli cha Usaliti** © Nyamari M. Abel

Imechapishwa kwa mara ya kwanza 2023

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya mwandishi na/au wachapishaji.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume cha sheria ataweza kushtakiwa.

ISBN 979-8654-15-500-7

---

Imechapishwa na Kuchapishwa na Elong'o Publishers

Nairobi, Kenya

Barua pepe: info@elongopublishers.co.ke

Simu: +254742433826

Tovuti: https://elongopublishers.co.ke

# TABARUKU;

Riwaya hii naitabaruku kwa mamangu Dorcas Nyamari, babangu Fredrick Nyamari pamoja na ndugu zangu; Mathew Nyamari, Claudia Bisase na Lewis Nyamari kwa kuwa nguzo kuu katika aushi yangu. Pia naitabaruku kwa mke wangu Claire Kaenga kwa mapenzi ya kipekee anayonipa, na mwanangu Noelle Kimberley kwa kuleta faraja akrabani. Kama akraba ya kipekee, Mola awatunuku maisha marefu yenye nakshi na awape stara daima dawamu.

# Yaliyomo

TABARUKU; .......... iii

SURA YA KWANZA .......... 1

SURA YA PILI .......... 6

SURA YA TATU .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA NNE .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA TANO .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA SITA .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA SABA .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA NANE .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA TISA .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA KUMI .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA KUMI NA MOJA .......... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA KUMI NA MBILI .......... **Error! Bookmark not defined.**

SHEREHE .......... **Error! Bookmark not defined.**

# SURA YA KWANZA

Maua yenye rangi tofauti tofauti yaligeuza sehemu ile ya mavani kuwa bustani zuri la kupendeza na kutamanika kwa kiasi kikubwa. Utulivu wake ulimfanya yeyote aliyekuwa pale awaze na kumliwaza kwa ndani kwa starehe zake na kujiona kiumbe pekee cha thamani duniani. Mathalan, vipepeo wenye madoadoa ya kupendeza walitua kutoka ua moja hadi jingine kwa madaha kama wanamapambo wa harusi ya Bi. na Bw. mkubwa. Mandhari haya yalifikishwa upeo na sauti tamu tena nyororo za chini zilizotolewa na wale nyuki waliofyonza mbochi, sauti zilizokwenda sawia na bendi za watiribu jukwaani. Milio ya kila aina ya ndege ilienda sambamba na zile ala za muziki mwororo wa kuliwaza. Makaburi meupe sampuli ya theluji yalilazwa pale yakiwa yamepangwa kwenye mlolongo kama gwaride la jeshi la maji. Kila kaburi lilikuwa na msalaba uliochomoza juu na maandishi machache kumhusu mwendazake.

Katika kaburi moja kwenye sehemu ya msalaba, kulikuwa kumeandikwa, “Padri Stefano 1935 – 2010” kisha maelezo fulani yakafuata chini yake. Ikiwa ni asubuhi kama yoyote ile ya kawaida, binti mmoja aliyanyunyizia maji maua yaliyozunguka kaburi lile kabla ya kuzuru kaburi jingine kwa zoezi hilo. Mara aliuondoa utando ambao buibui walikuwa wamejenga usiku kucha katika shughuli zao za mawindo. Aliona jinsi tu wadudu wengine walivyonaswa katika utando huo ndivyo binadamu wasio na hatia humalizia kujinasa katika mitego ya maadui na hatimaye kumezwa na ulimwengu uliojaa ukatili. Kamwe, hakuona kinyongo chochote katika kazi yake ya kila asubuhi. Hivyo ndivyo Salima Habibu alivyokuzwa. Aliambiwa lazima angeitunza nyumba ya watakatifu waliotangulia kama njia ya kupata ustawi na neema za kila siku.

Salima kwa wakati huu alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili, bado yeye ni kigoli, ndipo kumalizia awamu yake ya utoto na kufungua ukurasa wa ujana. Hata hivyo alifahamu namna ya kuzilaza nywele zake ndefu nyeusi ti (za singa) kwenda nyuma na kuzifunga julfa. Uso wake wa ngozi nyororo ya kinjano uliokosa alama na kutunukiwa vidu kwa mashavu ulimpa sura ambayo ni adimu kuonekana ulimwenguni. Macho yake malegevu yaliyosharabu weupe, yenye huruma na mboni nyeusi yalilindwa imara na kope laini za kumetameta. Mwone jinsi aliovyoumbika. Msichana aliyeumbwa akakamilika. Hana kasoro wala kovu

lolote, utadhani aliumbwa kwa upendeleo. Meno yake yaliyojipanga kinywani kama lulu katika chaza. Msichana aliyetunukiwa na vidu alivyojua namna ya kuvitumia kwa lile tabasamu lake la kulazia. Kwa kweli Salima alikuwa zaidi ya ua zuri lisilokinaisha kutamanika. Hata wale waliokuwa mavani ni bayana kwamba walitosheka na huduma za kiumbe hiki kilichowajali, wakataka aendelee tu kuwatunza milele.

"Salima! Salima!" Iliita sauti moja ya mwanamke kutoka upande wa chini kwenye kiingilio cha mavani. Alikuwa ni mwanamke aliyevalia nguo ndefu ya hudhurungi iliyochukua mtindo wa sare. Nywele zake daima hungeziona kwani alizifunika kwa kilemba cheupe kirefu hadi mabegani. Haikosi huyu ni bikira. Alizoea kuitwa 'sista' kama mabikira wengine walivyoitwa. Alikuwa ni Sista Joyce aliyekuwa kama mama wa kambo kwa Salima. Salima alimpenda na kumkubali Sista Joyce kama mama mzazi kwani alimpa malezi mema na wasia wa busara nyingi. Mara si moja, Sista Joyce alijizuia kumjuza Salima yaliyompelekea kujipata mikononi mwake. Alimwona mchanga kufahamu makuu na mazito ya ulimwengu. Hata hivyo aliona muda ulikuwa umewadia wa kumpasulia mbarika.

Sista Joyce alimpata Salima akiwa kwa kaburi lile la Stefano ameyoyomea katika ulimwengu wa ruiya na maono. Salima anapotulia hapa huwa anawaza sana na moyo humpiga kwa kasi. Alikumbuka uchangamfu wake Stefano na uhalisia aliokuwa nao katika mahubiri yake. Daima hangekosa kuhudhuria misa zake kwa vile alijihisi kiumbe kipya baada ya ibada zake. Padri Stefano alikuwa mkarimu sana tena mwenye upole. Baada ya kutamatisha misa, watoto wangemkimbilia ili awashike vichwa naye akatamka maneno fulani, wakaenda nyumbani wakiamini amewabariki. Wakati mwingine angeingia katika madarasa ya dini, akawazawidi maziwa ya pakiti kila mmoja hadi Sista Joyce, mwalimu wao wa dini.

Kifo chake kiliwaacha wengi wakiwa wamepigwa na butwaa. Alikuwa akiugua ugonjwa wa saratani ya figo kwa muda mrefu hadi pale mauti yalipomwatua moyo. Hata wahudumu wa hospitali ya misheni ya St. Agnes walihisi kutoweka kwa mtu wa watu. Lilikuwa ni pigo kubwa kwa wengi wa wafuasi wake hasa kwa Salima Habibu aliyempenda na kumthamini hadi mwisho. Wasemao husema kwamba chema hakidumu kwani wale wanaostahili kuishi sana ndio hufa. Salima alijitolea kutunza malazi yale ya milele ya Stefano. Wakati mwingine kibaridi chepesi kilichoandamana na upepo kilimpiga na kuona kiwiliwili chake Stefano

kikitokomea hewani. Aliona ni kama Stefano alitaka kumfahamisha suala fulani lakini tena akasita. Kila wakati kiwiliwili cha Stefano kilipopotea, ndipo Sista Joyce alijitokeza. Ni kana kwamba kilienda kumwita naye akaitikia mwito.

Sista Joyce alikwisha msoma Salima na kutambua kilichokuwa kikimsunza. “Mwanangu, mauti ni hatima ya kila mja, na chochote kinachoona mwanga hakina budi kuonana na kiza. Ni mlango ambao kila mmoja atapitia siku zake zinapofika, apende asipende. Mauti hayahepukiki na sisi sote tu safarini. Kama ilivyo desturi, kila safari ina mwisho wake. Stefano amekwisha kutamatisha yake. Sasa ni awamu yetu kuzifanya safari zetu kuwa nyoofu tena safi. Kadri siku zinapokwenda ndipo tunavyopiga hatua kufika ukingo wetu.” Maneno yake Joyce yalikuwa ya kutuliza mno japo ya kutamausha. Alimshika Salima begani naye akaangusha uso.

Sista Joyce alimkagua Salima kwa ukaribu. Aliona kweli amefika umri wa kufanya maamuzi makomavu. Salima alikuwa ameanza kunenepa kiuno na kifua chake kilianza kuinuka japo si sana na kusimama imara kuwili kama miba ya mkonge. Salima alikuwa bado hajielewi naye Sista Joyce alifahamu hilo. “Salima! Mwanangu, nataka unisikilize na kunipa makini. Nimekuwa nikijiuliza ni lini; lakini wewe sasa u mzima. Nimeona ni heri nikujuze mengi usiyoyafahamu.”

Kweli alitaka kuyafahamu mengi. Mengi ambayo ametamani kuyajua ingawa alitiwa subira ambazo aliona hazivuti heri. Mara si moja amekuwa akitaka kufahamu mengi lakini Sista Joyce akajitia hamnazo. “Mwanangu, wewe bado mtoto wa kufahamu makubwa. Mambo mengine yamekupiku; ni heri uhepukane nayo la sivyo yatakusunza bure.” Hivyo ndivyo alivyojibiwa kila mara alipomtolea dukuduku lililokuwa moyoni mwake. Salima alichoka kusubiri chambilecho ndimi za wahenga; ngoja ngoja huumiza matumbo.

“Stefano ndiye alikuleta hapa kwetu Kigombo kwa masista tukulee. Wewe ulikuwa mchanga mno, hukujijua wala kujielewa. Baada ya kulemewa na uzazi na kushindwa kukabiliana na ukatili wa ulimwengu, mamako, Bi. Tanya, aliona heri nusu shari akakukabidhi kwake Padri. Najua humfahamu ingawa ulionja titi lake. Ulimwengu ulikuwa umemwonyesha kasumba za kutosha. Hakutaka kamwe uyapitie maisha magumu aliyoyapitia. La! Alitaka ulelewe kwa misingi ya kidini na uwe mcha Mungu. Ndoto yake itatimia pale ambapo wewe utafikia uamuzi wa kuwa sista.” Maneno haya yalimwingia Salima bongoni na kumshika

mshipa wa hisi. Huo ndio ukweli mchungu ambao hakuufahamu na daima aliishi kutamani kujua.

Aligeuka na kumtazama Sista Joyce kwa macho yaliyojaa hisia kali. “Sista! Nina mama? Nimekuwa nikidhani kwamba sina mama. Labda nikaonewa imani na kuokolewa kutoka mapipani na kuletwa hapa. Mbona aniasi na, unamfahamu unijuze?” alitamani sana kujua. Alitamani amwone na kumkumbatia, ampe pole hata kama hakumkosea.

“Kwa sasa hilo ni gumu na sina habari yoyote hata kumhusu mamako. Labda tukaulize mzuka wake Stefano. Mwongo mmoja umepita bila kusikia lolote kutoka kwake.” Sista Joyce alimjibu. Hayo siyo Salima alitaka kujua kwa wakati huu wa kupasuliwa mbarika. “Na baba je? Sina baba? Mama alipitia dhiki gani hizi za kusalimu amri ya kunilea?” Salima alikuwa mwingi wa maswali lakini Sista Joyce alikuwa na kauli moja tu, “hayo yote Stefano angetujuza angelikuwa hai.”

Salima alisononeka sana kupashwa habari hizi. Hata kama alimpenda na kumthamini Sista Joyce kama mama mlezi, mama pekee aliyemjua, alitamani atoke siku moja na kutokomea mbali kabisa kumtafuta Tanya. Ni leo hii amejua jina la mamake kwa mara ya kwanza. Sista Joyce hakuwa mbaya. Alimlea Salima kama mzazi wa kweli tena mwenye mapenzi kwa mwanawe. Alifahamu vyema kwamba katika aushi yake ya ubikira hatakuwa na fursa ya kupata mtoto na hivyo akajituma zaidi katika malezi ya Salima.

Sista Joyce alikua na ndoto ya kumwona Salima akimaliza masomo na kuwa bikira kama yeye. Kwa kuwa bikira, aliona atakuwa wa manufaa kwa wengi na pia atahepukana na mikasa ya ndoa kama ile aliyopitia Tanya. “Salima mwanangu, Tanya alitaka uishi maisha mazuri. Stefano pia alikutakia maisha mema. Maisha mazuri ndiyo tunakutakia sisi. Uwe bikira. Uitwe sista. Sista Salima. Mwenye mienendo sawa na maadili ya kupigiwa mfano. Mwenye manufaa kwa wengi na kuwaongoza kwa njia ya haki na ukweli. Uwe nuru kwa waliopotea gizani,” aliishi akimpa mwongozo na mawaidha.

Wakati mwingine alimhepusha na macho ya vijana waliokuwa wanammezea mate. Ungewaona vijulanga wakiwa wanapiga kambi kwa ua la nyumba za masista, vichwa vyote vikigeukia nyumba ya Sista Joyce, ungedhani ni mazoezi ya makurutu. Sista Joyce alipowagundua, aliwafokea vikali nao wakachana

mbuga miguu niponye. Lakini kwa vile tabia ni mazoea, hawakukoma kamwe kupiga kambi uani mwa masista. Wanasayansi husema ua la kung'aa haliachi kuwavutia nyuki, naye Salima alikuwa ua la kipekee machoni mwa wengi!

Salima akiwa na umri wa miaka kumi na miwili alisomea shule ya wasichana ya misheni ya St. Andrew's. Shule hii ilikuwa ya bweni kuanzia wanafunzi wa darasa la nne. Hata hivyo, mara mojamoja, waliruhusiwa kutoka nje wakati maji yaliisha shuleni na kwenda kuteka bwawani. Kila Jumapili, waliruhusiwa kuhudhuria misa za kanisa la St. Andrew's ambalo lilikuwa maili chache tu kutoka shuleni. Wakati wa likizo wanafunzi wengine walipokwenda makwao, Salima alienda kwa masista maana hapa ndipo alipopachukulia kama kwao. Hata kama Kigombo palikuwa nyumbani pa malezi, alitamani naye awe na mahali kwingine pa kuita nyumbani. Nyumbani kwa mama labda. Kwa njia moja au nyingine, Salima aliapa liwe liwalo siku moja atatoka, aende kuitafuta familia yake na kuikubali hata kama angeipata ikiwa imevunjikavunjika. Asitake hata kujua ni kwa namna gani atampata Tanya, lakini amtafute bila kuchoka. Hata hivyo ilikuwa ni vigumu sana kwani hakujua aanzie wapi ikizingatiwa hakumfahamu Tanya, babake wala ndugu zake ikiwa walikuwepo.

Salima hakutaka kusomea shule ya upili ya karibu endapo angefaulu mtihani wa shule ya msingi. Alitaka asomee mbali na Sista Joyce, apate uhuru wa kujisimamia na kutangamana na wengine, fursa ambayo alinyimwa na Joyce. "Mbona bikira asitangamane na wengine? Ni utu asio nao ama ni kosa la usaliti wa dini?" aliishi akiwaza. Hakufahamu katu kwa nini Sista Joyce alimkanya kutangamana na wengine. Labda hakutaka wampotoshe kwani aliusibu msemo; dudu liumalo silipe kidole. Kule kwa Masista, aliruhusiwa kutangamana na wasichana wengine ambao pia walisomea dini. Kathra alikuwa rafiki wake wa karibu japo alikuwa darasa moja nyuma ya Salima. Yeye aliishi kwa Sista Hope.

Kujua ukweli kulimnyima amani na kumpa uchovu wa ghafla. Alifahamu sasa yale Stefano alitaka kumjuza kwa kile kiwiliwili chake. Si bure Salima huhisi mtulivu mno anapokuwa mavani. Alitoka kule kichwa kikiwa kimemjaa mawazo na fazaa tupu. Sista Joyce alijipata katika hali ya vuta nikuvute ya kifikra, ajutie kwa kumpasha ukweli ule ama ajihisi huru kwa kutenda haki. Haki iliyokuwa ikimsuta kila mara kama kikohozi kilichomkwama kooni. Jua lililokuwa limechomoza lilianza kushika makali nao upepo ukawaandama kana kwamba ulikuwa unawaambia, "Nendeni kwa amani enyi watakatifu wenye mapenzi mema!"

# SURA YA PILI

Bwana Balaa Beluwa aliegemea kwenye kiti chake cha bembea kilichotengenezwa kwa miti ya kupindwa nje ya jengo lake, mkono mmoja ukiwa umekamata kidevu nayo macho akayatunga angani. Tangu atoke ughaibuni hivi majuzi, maisha yamekuwa yakimwendea upogo. Siku ile alipotoka ng'ambo na kutua viamboni Kigombo, habari za kuwasili kwake ziliwapata wengi kwa kishindo. Hamna aliyemtarajia arejee hata kumtaka arejee baada ya kuvuka ng'ambo. Walikuwa wamemtia katika kaburi la sahau na kumtupa na vitimbi vyake. Alipohamia ughaibuni, wengi walitoa shukrani kuntu na kumshukuru Mola kwa kujibu dua lao na kuwaondolea kizungumkuti kilichokuwa kero na kuwafika kooni. Alikuwa amekuwa kero kwa wengi, akawakera na kuwakereketa maini.

Siku alipowasili, Balaa Beluwa aliandamana na binti mmoja chotara aliyekuwa na sura ya kizunguzungu yenye chembechembe za kiafrika. Mabinti wa aina hii wanafahamika kwa sana kama *Black Americans*. Binti huyo alipendelea mtindo wa kuvalia sketi fupi aina ya mini na suruali ndefu iliyofika hadi kisiginoni kutoka ndani. Kisha alivalia blauzi fupi ambayo ilikusudiwa kuwa kanchiri lakini yenye mikono mirefu ya vifungo. Blauzi hiyo haikutimiza jukumu lake kikamilifu kwani iliwacha vilima viwili vilivyotengana vikichungulia kutoka juu. Kitovu kilibaki hadharani labda kuonyesha kipini cha shaba kilichoninginia kwacho. Kope za kitana na nywele zake nyeusi za kusuka zilizoyumbayumba alipotembea zilichukuana na miwani mieusi iliyotulia machoni na juu ya kipua chake. Viatu vya mchuchumio vilimfanya atembee kama aliyekuwa katika maonyesho ya urembo. Mabinti kama huyu ni adimu kuwapata njiani, ila kwa filamu. Kati ya warembo wote wanaotambulika, Kamaria Fasihi ndiye alikuwa mbele kama mfuko wa shati. Kwa kifupi alifahamika kama Fasihi.

Balaa alimkamata Fasihi kiganjani akivuta begi lililokwenda kwa vijigurudumu vidogo huku nyuso zao zikionyesha furaha ya kutua nyumbani pageni. Watu waliwakaribisha tu kwa macho ya miondoko. "Mwone sasa! Baada ya kumpa

talaka mkewe na kwenda ng'ambo, ameamua kumwoa msichana rika ya watoto wake. Aibu hii!" Watu hawakuacha kusema.

Kwa kweli walitembea pamoja kama pea ya kiatu cha kiume kwa cha kike. Watu walijitia tayari kupokea vioja kwa msimu mwingine. Hawakukumbuka uzuri wake japo mchache. Hata nyimbo na mashairi aliyowakariria ya kutumbuiza akiwa mlevi hawakuyakumbuka. Ni bayana kwamba baniani mbaya kiatu chake dawa lakini kwao kiatu chake hakikuwa dawa bali sumu. Walikumbuka tu namna alivyolewa chakari na kuenda haja katika kibwawa walichokitegemea kuteka maji, jambo lililowafanya wanakijiji kuchunga kibwawa hicho kama kasri wakawa wanamfumania kwa mijeledi babamtu alipoyumbayumba kwenda kule kukilaki na kutoa kombora za matusi kwa wanakijiji. Balaa hakuwa wa kusikia bee wala tee, akawa hakanyiki na kila mara akiwa amelewa alikwenda kukisalimu kibwawa kile. Kibwawa kile kiliitwa kibwawa cha Chipuka. Tangu kufika kwake, Fasihi amekuwa riwaya mpya ya kusimuliwa mtaani.

Akiwa ameketi kule chini, Balaa alitafakari kwa mapana na marefu. Wasemao husema kumbukumbu ni hazina isiyoweza kufutika. Akili yake iligeuka kiwanda cha tafakuri akakumbuka vyema siku ile alipojiwa na Bamba Makini. Bamba alikuwa nduguye Balaa, kifunguamimba. Alifanya kazi ya uhandisi katika kampuni moja iitwayo *Royal Metal Manufactures* iliyo na makao makuu pale ng'ambo Minnesota, Marekani. Balaa alimfuata Bamba. Alifanya kazi katika kiwanda kimoja cha kukarabati magari. Visa vya uporaji wa vifaa maalum vya gari vilipozidi, alikuwa miongoni mwa wale walioonyeshwa mlango. Baada ya kupiga kiguu huku na kule kutafuta riziki kwingine, kwa bahati ya kipekee alifanikiwa kuajiriwa katika shirika moja linalosimamia uuzaji wa vipuli vya magari. Aliwekwa kama msimamizi mkuu wa fedha za uagizaji wa vifaa hivyo. Shida hazikukosa kumwandama kule aliporipotiwa kwa kosa la kununua vifaa ghushi na shirika likaanza kufilisika. Alipigwa kalamu na kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili gerezani.

Pamela Bopo ndiye alimfuata Balaa Beluwa tena kifungamimba katika familia hii ya Pengo Mapengo. Yeye alikuwa nesi katika hospitali moja ya kibinafsi kule Mtito Andei. Katika ndoa yake, hakufanikiwa kupata mtoto wa kiume hata mmoja. Alirejelewa kuwa tasa kwa kutojaliwa mtoto wa kiume kulingana na mil ana desturi za jamii yake. Alikuwa na wasichana watatu, mmoja akiwa shule ya upili na wawili katika shule ya msingi. Wanawe hawakuonyesha ukaidi wowote

wala utovu wa nidhamu. Walikuwa kielelezo chema cha kupigiwa mfano katika jamii.

Baada ya kumaliza kifungo chake, alionekaniwa na nyota ya jaha. Kwa vile undugu ni kufaana tena damu ni nzito kuliko maji, Bamba alitia fora kule ng'ambo na kumtafutia kibarua kingine. Kwa vile alifahamu Balaa amebobea katika sekta ya ukarabati wa magari, alifanikiwa kupata nafasi katika kampuni moja ya *Pan- Auto Link* iliyotopea katika uundaji wa vifaa vya kudumu. Hili lilikuwa jambo la mwisho Balaa alitarajia kutoka kwa nduguye. Ukame wa hela aliokuwa nao ulikuwa umemfikisha ukingoni akawa maskini asiye na mbele wala nyuma. Alipewa fursa murua ya kuvuka ng'ambo na ayali yake, akaipokea fursa hiyo kwa mikono miwili ingawa aliingiwa na kiburi.

Wiki tatu kabla ya kung'oa nanga kwenda Minnesota Marekani, Balaa alifanya maamuzi ya dharura. Alimsihi Bamba amruhusu waondoke naye bila kuandamana na familia yake ilivyoazimiwa. Kisa na maana, aliona mkewe hatamfaa katika shughuli zake kule Minnesota tena atamharibia nemsi yake, akamwona akiwa zuzu asiyewezana na maisha ya uzunguni. Balaa alitaka aionje, ainywe na kuila raha peke yake tena mbali na akraba yake. Mara si moja alikuwa amedokezewa kuwa Marekani kulikuwa na maisha mazuri hivyo kuandamana na familia kungemhini uhuru zaidi aliotaka kubugia.

Awali, Balaa alikuwa mwenye mapenzi tele kwa familia yake changa japo mienendo yake kazini ilikuwa mibovu. Alipopata fursa ya kusafiri nje, alifichua makucha yake – alikuwa tai aliyejifunika kwa manyoya ya hua. Alikiuza chochote kile kilichoweza kuuzika na kubeba chochote kile cha thamani. Talaka ya ghafla aliyompa mkewe ilimwathiri Tanya nusura aambulie wehu.

Usiku huo kabla ya kuondoka na kuabiri ndege ya asubuhi, Balaa alimpasulia mkewe mbarika ya kutoandamana naye. Mkewe hakuamini aliyokuwa akiambiwa, akashtuka hadi ya kushtuka akawa sasa hamwoni yule Balaa aliyemfahamu bali ibilisi wa Balaa. Ile tamaa na ari ya kwenda ughaibuni ilimkwisha ghafla akatawaliwa na fazaa tupu. Alijaribu kumsihi na kumshawishi kwa namna zote amruhusu waandamane naye kama alivyomwahidi awali lakini Balaa akakataa kata kata. Alikaidi kama mkia wa mbuzi kikawa ni kilio kwa mwamba upasuke maji. Kitoto chao hakikujua kilichokuwa kikiendelea, kilikimya tu, kikakodoa macho na kufurisha mashavu kama andazi.

"Ikiwa wewe ni wa kusikia na basi nataka usikie. Kule ughaibuni nakwenda kazi si malezi, sina budi kuondoka nikakuacha hapa. Usidhani maisha ni mazuri pale kuliko hapa. Kumbuka wa kusaidiwa huonyesha moyo. Sikuwa na hela, hali inayonipelekea kupiga seli nyumba hii angalau niondoke na senti zangu. Hamna chetu humu, nishapiga kila kitu seli. Itakulazimu utafute pa kujisitiri kwa muda." Hayo ndiyo yalikuwa matamshi yake Balaa. Aliyasema kwa ufasaha ungedhani alikuwa amefanya matayarisho na kuyapiga msasa. Hivyo ndivyo masikini wa watu Bi. Tanya alivyosalitiwa na kuachwa na kitoto chake kisicho na hatia, Salima Habibu, kumenyana na ukungu wa ufukara uliowasubiria.

Balaa aliabiri ng'ambo hatimaye. Asubuhi hiyo haikuwa ya kawaida kwake Tanya. Wenye mali walisomba kila kilichokuwa mle. Aliwatupia tu macho ya huruma yasiyowazuia wenye mali waliozidi kunyakua hata kisicho chao. Mwishowe, nyumba nzuri ilisalia ikiwa imesimama bila chochote ndani, yeyote aliyeiona kutoka nje aliitamani kupindukia lakini pindi aingiapio ndani umwone akitoka kama yule aliyeingia kuzimu. Kulikuwa na utulivu wa aina yake ambao ulisheheni mengi makuu yasiyoelezeka.

Kule Marekani, Balaa hakuchukua muda kabla hajampata mchumba. Alifanya kazi ya uchukuzi na usafirishaji wa vifaa vya gari kutoka kwa kampuni hadi marikiti au kwa wateja. Kazi hii hakuiona ikiwa ngumu kwani ilimhitaji pale tu alipohitajika kusafirisha. Muda mwingi aliutumia kupiga soga na wafanyakazi wengine. Hivyo ndivyo alivyotangamana na Regina, mweka hazina katika shirika lile la *Pan-Auto Link.*

Regina alikuwa mwanamke aliyefikia umri wa kuolewa lakini bahati yake ya kuolewa haikuwa imesimama. Labda ni kutokana na muda mwingi aliotumia afisini uliomhini nafasi ya kutambulika na kutamanika ama kutokana na cheo chake kilichomfanya aonekane kama mwanamke mwenye hela nyingi ambaye si rahisi kufikiwa. Regina alikuwa mweupe wa uzungu wa kweli. Matendo yake afisini yalionyesha wazi kwamba anamtongoza Balaa. Regina alivaa mavazi yaliyombana sana na kuketi kiholela hajali wala habali utadhani hakuumbiwa aibu. Mara nyingi utampata afisini akiwa amekuda sketi yake huku akijipa shughuli zake. Miguu yake ilikaidi kutulia pamoja, mmoja utakuwa hapa na mwingine kule, mwenye pazia ayafunge macho yake.

Endapo hakuwa ametenganisha miguu ovyo, chuchu zake zilichungulia kutoka sehemu ya juu ya kanchiri iliyombana ikafunikwa na blauzi ya kubana. Kifua hiki

ni kama kilikuwa na sumaku kwani Balaa aliishi kuyatunga macho pale na kukitazama bila soni. Alipomwambia, "*Today you're looking gorgeous!*" Regina alitoa tabasamu la kulazia na kumjibu, "*Seriously? I appreciate!"* Hayakuishia hapo. Regina aligeuza mtindo wake wa kutembea pindi tu alipomwona Balaa akimwangazia. Alitembea huku akitikisa kiuno kama nyuki aonapo mbochi, mkono mmoja ulikamata kifuani na mwingine ukaninginia hewani kwenda juu kama mguu wa mbele wa kangaruu.

Balaa alihitaji kutia chudi kiasi na azma yake ingeafikiwa. Naye kama sonara asiyekosea katika ufundi wake, alijituma. "Regina? *You are fabulous. Shall we?... Maybe a cup of coffee?"* Alimwambia siku moja alipoona hali yake haimpi muda wa kuipoza. "*Sure*." Alimjibu kwa izara. Jioni ya usiku huo walifika katika hoteli ya West Park, Balaa akadhihirisha kwamba yeye ni jogoo anayewika shambani na mjini. Tangu hapo, wawili hawa walijitangaza kuwa wachumba. Ulikuwa ni mwanzo mpya wa Balaa ambaye alikuwa na bahati ya mtende kumpata mpenzi ambaye amekuwa akitamani tangu ahamie ughaibuni.

Utamu wa maisha ulizidi kule ng'ambo. Alimsahau kabisa mke wake wa awali, Tanya, aliyemwacha hohehahe na kukimbilia anasa za ughaibuni. Halikuwahi kumjia wazo kuhusu hali ya maisha ya Tanya wala Salima Habibu, mwanawe wa kwanza. Alikuwa ametiwa kifungamacho haoni wala kubashiri. Tanya aliachwa kupambana na ulimwengu mkavu. Alijaribu maisha kutoka kila upande lakini pande zote zikawa hazimpi matumaini. Aligeuzwa na kuwa mke wa kuhuni na kuazima vya bure. Shamba lao la miti ya kuchoma makaa ya kuuza lilikuwa limeuzwa na Balaa kwa tajiri mmoja aliyeligeuza kuwa shamba la pamba. Darahima kidogo alizokuwa nazo zilimezwa na mahitaji ya Salima. Waliompa msaada walianza kumdai madeni yao, machache akayalipa kwa kukopa kwingine lakini iwe hivi hadi lini? Hamna biashara ambayo hakuipa majaribio hata kama ni uhuni. Si kibarua cha kulima makondeni wala si kuwatekea watu maji. Wasemao husema mshoni habagui nguo. Maisha yalimwia magumu akaingiwa na mashaka na tuhuma moyoni mwake.

**JINYAKULIE NAKALA ILI UENDELEE KUSOMA**